

**PAROKIA YA MT. MARIA DE MATTIAS-MIVUMONI
DAR ES SALAAM**

**MATANGAZO YA DOMINIKA YA TANO YA PASAKA
MWAKA B TAREHE 28/04/2024**

MCHANGO WA PILI

Mchango wa pili kwa ajili ya **SAMANI ZA OFISI**. Jumuiya inayohudumia iandae vyombo. Kwaya mtuongoze kwa wimbo.

TANGAZO LA NDOA

Bw. Stanley Chali mtoto wa Focas John na Cesilia Thomas na Bi. Jesca Lameck mtoto wa Japhet Bahena na Leonia Emmanuel.

Bw. Fabian Endward mtoto wa Endward Neye na Felista Lugeza na Bi. Lucia Mahajile mtoto wa Andrea Masumbuko na Auleria Maselebu.

Bw. John Valerian mtoto wa Valerian John na Bertha Obed na Bi. Irene Emmanuel mtoto wa Emmanuel Nkumbi na Regina Kisoli.

Bw. Erastus Mgombera mtoto wa Peter Mgombera na Consolata Mhoma na Bi. Maria Amiri mtoto wa Amiri Salumu na Nunu Said.

Tangazo la kwanza.

Bw. Deusdediti Amani ya Bwana mtoto wa Danieli Mashinga na Basilisa Kilanamshari na Bi. Genovefa Mkabahati mtoto wa Akwilin Hassani na Emerensiana Mkameli.

Bw. Nathanael Mwasenga mtoto wa Emmanuel Mwasenga na Elizabeth Mwambogo na Bi. Devota Mzumbwe mtoto wao Simon Zubeli na Rehema Edward.

Tangazo la pili.

Bw. Tonny Albert Kitumbo mtoto wa Albert Kitumbo na Helena David na Bi. Dorren Elisaria Massawe mtoto wa Happymack Silayo na Hazelina Mrema. **Tangazo la tatu na la mwisho.**

Anayejua kizuizi chochote cha matangazo haya atoe taarifa ofisi ya Mapadre.

PUGU MARATHON

Kamati ya Pugu Marathon chini ya usimamizi wa UWAKA na WAWATA inawataarifu kuwa Pugu Marathon 2024 itafanyika tarehe 18 Mei. Ufunguzi rasmi wa Marathon hii umefanyika na Askofu Mkuu katika mkutano na waandishi wa habari, hivyo unaweza sasa kujisajili katika tovuti ya jimbo www.jimbodsm.com kisha kulipia kupitia mitandao ya simu. Malengo ya mbio hizo ni kuendeleza kituo cha hija Pugu, matendo ya huruma katika hospitali na wahitaji, kuhamasisha mazoezi kwa afya. Kwa maelezo zaidi onana na uongozi wa UWAKA Parokia.

TANGAZO LA MOYO MTAKATIFU WA YESU

Wana Shirika wa Moyo Mtakatifu wa Yesu wanamshukuru Mungu kwa Uinjilishaji uliofanyika Jana katika Kanda Ya Kapernaumu. Mwezi ujao wataendelea na uinjilishaji huo Kanda ya Kana.

TANGAZO LA UTOTO MTAKATIFU

- Watoto wanaendelea na mazoezi kwa ajili ya sherehe ya miaka 10 ya Parokia kila Jumamosi na Jumapili saa 10:00 Jioni hapa Parokiani. Tunaomba watoto wafike kwa wingi.
- Tunaomba Jumuiya ambazo hawajachukua fomu za mgawanyo wa matukio ya Utoto Mtakatifu ya mwaka mzima, watazigawa hapo nje ya Lango kuu la Kanisa mara baada ya Misa I na II. Baada ya hapo kwa wasiochukua watazikuta Duka la WAWATA.
- Watoto wataenda kurekodi kipindi Radio Tumaini siku ya Jumamosi ya tarehe 18/5, hivyo Watoto wanaendelea na maandalizi kwa ajili ya siku hiyo, kila siku ya Jumamosi na Jumapili saa 10:00 Jioni.

TANGAZOLA SHIRIKA LA MT. YOSEFU

Misa ya kupokelewa Wanashirika wa Mt. Yosefu itafanyika Dominika ijayo 5/5/ katika Misa ya kwanza.

BAHASHA ZA RADIO MARIA

Viongozi wa Jumuiya ambao hawajachukua Bahasha za Radio Maria mnaombwa kufika Ofsini mara baada ya Misa kuchukua Bahasha hizo.

KIKAO CHA WAZAZI NA WALEZI WA KOMUNIO YA KWANZA

Kutakuwa na Kikao cha Wazazi na Walezi wote wa Watoto wa Komunio ya kwanza Dominika ijayo ya tarehe 5/5 mara baada ya Misa ya Kwanza katika ukumbi wa Parokia. Mnaobwa kufika bila kukosa.

MISA YA IJUMAA YA KWANZA YA MWEZI

Kutakuwa na Misa ya Ijumaa ya kwanza ya Mwezi tarehe 3/5 saa 12:30 jioni, ikitanguliwa na Njia ya Msalaba, kuabudu na kuchoma maombi kwenye Grotto.

MISA KWA HESHIMA YA MAMA BIKIRA MARIA

Kutakuwa na Misa kwa heshima ya Mama Bikira Maria jumamosi ijayo tarehe 4/5 saa 3:00 asubuhi mara baada ya Sala za Jumuiya.

MATEMBEZI YA MSALABA

Leo Msalaba unakabidhiwa Jumuiya ya Mt. Martine De Porres. Dominika ijayo watapokea Jumuiya ya Mt. Faustina. Wakati huo huo Jumuiya ya Mt. Yohanne Vianney wajiandae.

MAUZO MBALIMBALI

Gazeti la Tumaini letu 1,000/=

HUDUMA KANISANI

Leo tunahudumiwa na Yohannes Sekondary School. Dominika ijayo tutahudumiwa na Jumuiya ya Mt. Petro. Wakati huo huo Jumuiya ya Familia Takatifu wajiandae.

SADAKA YA MATOLEO YA DOMIKA ILIYOPITA (Angalia kiambatanisho)

RIPOTI YA SHUKRANI 2023 & 2024(Angalia kiambatanisho)

BAHASHA ZA PASAKA

Waliorudisha bahasha za Pasaka karibuni mjongee mbele kwa baraka na kukabidhi bahasha.